

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS**

**Anuani ya Simu: "TAMISEMI"**

**Simu Na:** (026) 2322848, 2321607  
2322853, 2322420

**Nukushi:** (026) 2322116, 2322146  
2321013

**Barua pepe:** [ps@tamisemi.go.tz](mailto:ps@tamisemi.go.tz)



Tawala za Mikoa na  
Serikali za Mitaa,  
Jengo la Mkapa  
2 Barabara ya Hospitali,  
S. L. P 1923,  
DODOMA.

**Unapojibu tafadhali taja:**

Kumb. Na. AH.129/161/01/53

5 Oktoba, 2018

## TANGAZO

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI) inapenda kuwatangazia wahitimu wote wa kada za Afya nchini kuwasilisha maombi ya nafasi za kazi ili kujaza nafasi za waombaji waliochaguliwa awamu ya kwanza lakini hawakuripoti katika vituo vyao walivyopangiwa. Watumishi wataochaguliwa watapangiwa katika Halmashauri zilizopangiwa watumishi lakini hawakuripoti. Nafasi zinazotangazwa ni zifuatazo:-

- Daktari Daraja la II (Medical Doctor II)
- Tabibu Daraja la II (Clinical Officer II)/Tabibu Meno( Dental Therapist)
- Tabibu Msaidizi (Clinical Assistant)
- Afisa Muuguzi Darala la II (Nursing Officer II)
- Afisa Muuguzi Msaidizi Daraja la II (Assist. Nursing officer II)
- Mteknolojia Mionzi Daraja la II (Radiographer II)
- Fundi Sanifu Vifaa Tiba Daraja la II (Biomedical Engineering Techn II)
- Mtoa Tiba kwa Vitendo Daraja la II (Physiotherapist II)
- Mfamasia Daraja la II

## **SIFA ZA MWOMBAJI;**

1. Awe raia wa Tanzania;
2. Awe na umri usiozidi miaka 45;
3. Asiwe Mwajiriwa wa Serikali au asiwe Mwajiriwa wa Hospitali za Mashirika ya Dini ambaye mshahara wake unalipwa na Serikali; na
4. Asiwe amewahi kuajiriwa Serikalini nakupata check namba, na endapo itabainika kuwa alishaajiriwa, atatakiwa kuzingatia utaratibu wa uhamisho au kurejea katika Utumishi wa Umma baada ya kuacha kazi kama inavyoelekezwa kwenye nyaraka za Utumishi wa Umma za mwaka 2012.

## **MAOMBI YOTE YAAMBATANISHWE NA;**

1. Nakala ya cheti cha kidato cha Nne/Sita
2. Nakala za Vyeti vya Taaluma
3. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
4. Nakala ya cheti cha usajili kamili (Full Registration) au Leseni ya kufanya kazi ya taaluma husika
5. Maelezo binafsi (CV)
6. Picha (passport size 2) za hivi karibuni
7. Nakala za vyeti lazima vithibitishwe na Hakimu au Wakili

## **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI WOTE**

- Waombaji wote wawe tayari kufanya kazi Halmashauri yoyote atakayopangiwa
- Waombaji wote wawe tayari kufanya kazi na mashirika/taasisi zilizoingia ubia na Serikali
- Waombaji waliosoma nje ya nchi wanatakiwa waambatanishe pamoja na equivalent certificate kutoka NECTA/NACTE/TCU

Maombi yote yatumwe kwa njia ya mtandao (Online) kupitia mfumo wa kieletronic unaopatikana katika tovuti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Mwisho wa kupokea barua za maombi kwenye mfumo ni tarehe 12 Oktoba, 2018 saa 9:30 alasiri. Maombi yatakayotumwa nje ya mfumo hayatashughulikiwa.

**Tangazo hili linapatikana katika tovuti yetu**

[www.tamisemi.go.tz](http://www.tamisemi.go.tz)

**Imetolewa na; Mathew Kwembe**

**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano Serikalini  
Ofisi ya Rais – TAMISEMI,**

**5 Oktoba, 2018**